

Mwongozo wa Maombi ya Leseni ya biashara kwa Watoa Huduma Ndogo za Fedha bila kupokea Amana (Makampuni ya Kukopesha)

#### **A. Maelezo ya Jumla**

1. Mwombaji anatakiwa awe amesajiliwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni au sheria yeyote inayohusu makampuni
2. Jina la kibashara la mwombaji linatakiwa liwe na maneno yafuatayo "Microfinance", "Finance" "Financial Services" "Credit" au "Microcredit"
3. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya leseni ya shilingi 500,000 ambayo haitarudishwa
4. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi isiyorudishwa kwa njia ya uhamisho wa moja kwa moja wa TISS kutoka Benki zao kwenda Benki Kuu ya Tanzania  
Namba ya Akaunti ni: 9944713001  
Jina la Akaunti ni: MFCs & FICOs Application and Licensing Fees
5. Mwombaji atahakikisha ana mtaji usiopungua shilingi milioni ishirini pale anapoanza biashara na wakati wote.
6. Sera ya Mikopo ioneshe mambo ya msingi yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Watoa Huduma Ndogo za Fedha Wasiopokea Amana.

#### **B. Taarifa/Nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya Maombi ya Leseni**

1. Barua ya maombi kwenye fomu iliyoainishwa.
2. Hundi ya Benki au nyaraka nyingine yoyote inayokubalika na Benki inayothibitisha malipo ya ada.
3. Uthibitisho wa chanzo na upatikanaji wa mtaji unaopendekezwa na mtoa huduma ndogo za fedha.
4. Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya taaluma na utaalum vya wajumbe wa Bodi na Mtendaji Mkuu.
5. Nakala Taarifa za Fedha zilizokaguliwa hivi karibuni ikijumuisha mizania, taarifa ya mapato na mtiririko wa fedha wa mtoa huduma ndogo za fedha.
6. Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Namba ya Mlipa Kodi (TIN).
7. Sera ya Mikopo.
8. Uthibitisho wa idhini ya mamlaka ya udhibiti nchini kama mwombaji ni raia wa kigeni.
9. Tamko kwamba fedha itakayotumika kuwekeza haikupatikana kwa njia ya jinai au haihusiki na shughuli yoyote ya kijinai.

10. Uthibitisho wa uraia wa kila Mwanahisa na Wakurugenzi waliopendekezwa na Mtendaji Mkuu. Hii inajumuisha wasifu binafsi, picha mbili ndogo za hivi karibuni na mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:

- (i) Nakala ya hati ya kusafiria (passport) iliyothibitishwa, ambayo imebeba taarifa binafsi;
- (ii) Kitambulisho cha Taifa; au
- (iii) Cheti cha kuzaliwa

11. Dodoso lililojazwa kikamilifu kwa ajili ya Wakurugenzi, Mmiliki au Mtendaji Mkuu wa Watoa Huduma Ndogo za Fedha Chini ya Daraja la 2 lililoko katika Jedwari la nne katika kanuni

12. Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili wa kampuni.

13. Nakala iliyothibitishwa ya MEMART, Katiba au Masharti.

14. Maazimio ya Bodi yaliyoidhinisha maombi ya leseni.

15. Pale panapohitajika, orodha ya wanahisa au wajumbe wa Bodi na Mtendaji Mkuu.

16. Pale panapohitajika, taarifa ya kumbukumbu za mkopo kwa kila mwanahisa muhimu mwenye umiliki wa 5% au zaidi au mjumbe wa Bodi na Mtendaji Mkuu.

17. Pale panapohitajika, nakala zilizothibitishwa za hati safi ya kodi kwa mwombaji, mwanahisa muhimu au mjumbe wa Bodi na Mtendaji Mkuu.

18. Nakala zilizothibitishwa za marejesho ya mwaka ya hivi karibuni ya mtoa huduma ndogo za fedha.

19. Taarifa za Mtu wa kuwasiliana naye zinazoonesha Jina lake, Anuani ya Posta, Namba ya Simu na Barua pepe

20. Pamoja na nyaraka zilizo rodheshwa hapo juu, Makampuni ya nje yatatakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:

- (i) Mpango wa mafunzo unaoonesha muda uliotengwa wa kuwarithisha ujuzi wa Huduma ndogo za Fedha wafanyakazi wazawa
- (ii) Mpango wa kuwaandaa wafanyakazi wazawa kuchukua nafasi za uongozi katika Taasisi

*NB: Watoa Huduma ndogo za fedha walio katika Daraja la 2 linahusisha; Makampuni ya Kukopesha, Mashirika ya kifedha, makampuni ya kutoa mikopo midogo ya nyumba, Wakopeshaji binafsi na wakopeshaji wa kidijitali*